

**KUMB: PPR/16 - 3/1**

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI KIKOMO ZA MAFUTA AINA YA PETROLI KUANZIA  
JUMATANO, TAREHE 2 Machi 2016**

Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) inatangaza bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli hapa nchini. Bei hizi zitaanza kutumika kuanzia **Jumatano, Tarehe 2 Machi 2016**. Pamoja na kutambua bei kikomo za bidhaa mbalimbali za petroli nchi nzima, ni muhimu kuzingatia yafuatayo:-

- (a) Bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya aina zote yaani Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimebadilika ikilinganishwa na toleo lililopita la Februari 2016. Kwa Mwezi Machi 2016, bei za rejareja za Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimepungua kama ifuatavyo: TZS 31/lita sawa na asilimia 1.70, TZS 114/Lita sawa na asilimia 7.10 na TZS 234/lita sawa na asilimia 13.75, sawia. Vilevile, ikilinganishwa na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla kwa mafuta ya Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa nazo zimepungua kwa : TZS 34.36/lita sawa na asilimia 1.98, TZS 116.58/lita sawa na asilimia 7.80 na TZS 236.59/lita sawa na asilimia 14.84. Kwa kiasi kikubwa, kupungua huku kwa bei za mafuta kwenye soko la ndani kumetokana na kuendelea kushuka kwa bei za mafuta katika soko la dunia.
- (b) Hakutakuwa na mabadiliko yeyote ya bei za mafuta ya Petroli na Dizeli kwa mkoa wa TANGA kwa mwezi wa Machi. Hii imetokana na kutokupokea mafuta mapya kupitia bandari ya TANGA katika mwezi wa Februari 2016.
- (c) Mamlaka inapenda kuujulisha umma ya kwamba bei hizi kikomo za mafuta kwa eneo husika, zinapatikana vile vile kupitia simu za mkononi kwa kupiga namba **\*152\*00#** na kisha kufuata maelekezo. Huduma hii ni bure na inapatikana kupitia mitandao yote ya simu za mkononi hapa nchini.
- (d) Kwa mujibu wa Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta. Taarifa hizi zina lengo la kuwasaidia wadau kufanya maamuzi stahiki kuhusu manunuzi ya bidhaa za mafuta.
- (e) **Kampuni za mafuta zipo huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani mradi tu bei hizo ziwe chini ya bei kikomo (price cap) kama ilivyokokotolewa na formula iliyopitishwa na EWURA na ambayo ilichapwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 405/2015 la Mwezi Julai 2015.**
- (f) Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana na yakionyesha bei ya mafuta, punguzo, vivutio vya biashara au promosheni zinazotolewa na kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta kutoka kwenye vituo vinavyouza mafuta kwa bei ndogo zaidi ili kushamirisha ushindani. **Ni kosa kuuza**

**mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja na adhabu itatolewa kwa kituo husika.**

- (g) Wanunuzi wanashauriwa kuhakikisha kuwa wanapata stakabadhi ya malipo inayoonesha jina la kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hiyo ya malipo itatumika kama kidhibiti cha mnunuzi wa mafuta endapo kutajitokeza malalamiko ya ama kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei kikomo; ama endapo utakuwa umeuziwa mafuta yenye kiwango cha ubora kisichofaa.

#### **A: BEI ZA REJAREJA**

<b>Mji</b>	<b>Bei Kikomo</b>		
	<b>Petroli (Sh/Lita)</b>	<b>Dizeli (Sh/lita)</b>	<b>Mafuta Ya Taa (Sh/Lita)</b>
<b>Dar es Salaam</b>	1,811	1,486	1,465
<b>Arusha</b>	1,895	1,570	1,549
Arumeru (Usa West)	1,895	1,570	1,549
Karatu	1,913	1,588	1,568
Monduli	1,900	1,576	1,555
Ngorongoro (Loliondo)	1,951	1,627	1,606
<b>Kibaha</b>	1,816	1,491	1,470
Bagamoyo	1,822	1,497	1,476
Kisarawe	1,818	1,493	1,473
Mkuranga	1,821	1,496	1,475
Rufiji	1,839	1,514	1,493
<b>Dodoma</b>	1,870	1,545	1,524
Bahi	1,877	1,552	1,531
Chemba	1,896	1,571	1,550
Kondoa	1,902	1,578	1,557
Kongwa	1,867	1,542	1,521
Mpwapwa	1,871	1,546	1,525
<b>Iringa</b>	1,875	1,550	1,529
Kilolo	1,879	1,555	1,534
Mufindi (Mafinga)	1,885	1,560	1,539
<b>Njombe</b>	1,903	1,578	1,557
Ludewa	1,941	1,616	1,595
Makete	1,934	1,609	1,588
Wanging'ombe (Igwachanya)	1,901	1,576	1,555
<b>Bukoba</b>	2,026	1,701	1,680
Biharamulo	2,000	1,676	1,655

Karagwe (Kayanga)	2,042	1,718	1,697
Kyerwa (Ruberwa)	2,048	1,723	1,702
Muleba	2,026	1,701	1,680
Ngara	1,991	1,667	1,646
Misenyi	2,034	1,710	1,689
<b>Geita</b>	1,976	1,651	1,630
Bukombe	1,965	1,640	1,619
Chato	1,997	1,672	1,651
Mbogwe	2,014	1,689	1,668
Nyang'hwale	1,991	1,666	1,645
<b>Kigoma</b>	2,042	1,717	1,696
Uvinza (Lugufu)	2,054	1,729	1,708
Buhigwe	2,031	1,706	1,685
Kakonko	1,999	1,674	1,653
Kasulu	2,028	1,703	1,682
Kibondo	2,006	1,681	1,661
<b>Moshi</b>	1,885	1,560	1,539
Hai (Bomang'ombe)	1,888	1,563	1,542
Mwanga	1,878	1,553	1,532
Rombo (Mkuu)	1,905	1,581	1,560
Same	1,871	1,546	1,525
Siha (Sanya Juu)	1,891	1,566	1,545
<b>Lindi</b>	1,870	1,545	1,524
Kilwa Masoko	1,845	1,520	1,499
Liwale	1,891	1,566	1,545
Nachingwea	1,899	1,574	1,553
Ruangwa	1,897	1,572	1,551
<b>Babati</b>	1,933	1,608	1,587
Hanang (Katesh)	1,944	1,619	1,598
Kiteto (Kibaya)	1,944	1,619	1,599
Mbulu	1,946	1,621	1,600
Simanjiro (Orkasumet)	1,965	1,640	1,619
<b>Musoma</b>	1,989	1,664	1,643
Rorya (Ingirijuu)	1,998	1,673	1,652
Bunda	1,980	1,655	1,635
Butiama	1,986	1,661	1,640
Serengeti (Mugumu)	2,035	1,710	1,689
Tarime	2,000	1,675	1,655
<b>Mbeya</b>	1,918	1,593	1,572
Chunya	1,927	1,603	1,582
Ileje	1,931	1,606	1,585

Kyela	1,934	1,609	1,588
Mbarali (Rujewa)	1,902	1,577	1,556
Mbozi (Vwawa)	1,927	1,602	1,581
Momba (Chitete)	1,936	1,611	1,590
Rungwe (Tukuyu)	1,927	1,602	1,581
<b>Morogoro</b>	1,836	1,511	1,490
Mikumi	1,852	1,527	1,506
Kilombero (Ifakara)	1,874	1,549	1,528
Ulanga (Mahenge)	1,884	1,560	1,539
Kilosa	1,854	1,530	1,509
Gairo	1,854	1,530	1,509
Mvomero (Wami Sokoine)	1,846	1,522	1,501
Turian	1,861	1,536	1,515
<b>Mtwara</b>	1,883	1,558	1,538
Nanyumbu (Mangaka)	1,932	1,607	1,586
Masasi	1,909	1,584	1,563
Newala	1,915	1,590	1,570
Tandahimba	1,908	1,584	1,563
<b>Mwanza</b>	1,961	1,636	1,615
Kwimba	1,997	1,672	1,651
Magu	1,969	1,644	1,623
Misungwi	1,966	1,642	1,621
Sengerema	1,993	1,668	1,647
Ukerewe	2,020	1,695	1,674
<b>Sumbawanga</b>	1,983	1,659	1,638
Kalambo (Matai)	1,976	1,651	1,630
Nkasi (Namanyele)	1,997	1,672	1,651
<b>Katavi (Mpanda)</b>	2,018	1,694	1,673
Mlele (Inyonga)	1,997	1,672	1,651
<b>Songea</b>	1,934	1,609	1,589
Mbinga	1,968	1,643	1,622
Namtumbo	1,963	1,639	1,618
Nyasa (Mbamba Bay)	1,970	1,645	1,624
Tunduru	1,993	1,668	1,647
<b>Shinyanga</b>	1,940	1,615	1,594
Kahama	1,953	1,628	1,608
Kishapu	1,968	1,643	1,622
<b>Simiyu (Bariadi)</b>	1,981	1,656	1,635
Busega (Nyashimo)	1,974	1,649	1,628
Itilima (Lagangabilili)	1,984	1,659	1,638
Maswa	1,972	1,648	1,627

Meatu (Mwanhuzi)	1,979	1,655	1,634
<b>Singida</b>	1,901	1,577	1,556
Iramba	1,914	1,589	1,568
Manyoni	1,886	1,561	1,540
Ikungi	1,897	1,572	1,551
Mkalama (Nduguti)	1,926	1,601	1,580
<b>Tabora</b>	1,965	1,640	1,619
Igunga	1,919	1,594	1,573
Kaliua	1,983	1,658	1,637
Ulyankulu	1,977	1,652	1,631
Nzega	1,929	1,605	1,584
Sikonge	1,977	1,652	1,631
Urambo	1,978	1,653	1,632
<b>Tanga</b>	1,825	1,586	1,511
Handeni	1,846	1,607	1,491
Kilindi	1,861	1,622	1,525
Korogwe	1,838	1,598	1,504
Lushoto	1,847	1,608	1,514
Mkinga (Maramba)	1,832	1,593	1,526
Muheza	1,830	1,591	1,511
Pangani	1,832	1,593	1,518

**B: BEI ZA JUMLA**

Bei za Jumla - DSM	Petroli (Sh/L)	Dizeli (Sh/L)	Mafuta ya Taa (Sh/L)
<b>Bei Kikomo</b>	<b>1,702.97</b>	<b>1,378.22</b>	<b>1,357.39</b>

Bei za Jumla - TANGA	Petroli (Sh/L)	Dizeli (Sh/L)
<b>Bei Kikomo</b>	<b>1,720.47</b>	<b>1,481.29</b>

**Felix Ngamlagosi**

**MKURUGENZI MKUU  
EWURA**